

**MUHATASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA
KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI (REMP) TAREHE 28/10/2021
YENYE AGENDA MAALUMU YA KUJADILI FEDHA ZA MRADI WA UJENZI WA
MADARASA YA SEKONDARI, SHULE SHIKIZI, EMD NA NYUMBA YA MTUMISHI**

WATAALAM WALIOHUDHURIA

- | | |
|-----------------------|---------------------------------|
| 1. SALIM MSUYA | KAIM MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA |
| 2. AZIZI KITAMO | KAIMU AFISA UTUMISHI WILAYA |
| 3. SEBASTIAN GAGANIJA | AFISA MAENDELEO YA JAMII |
| 4. EMMANUELI MSUYA | AFISA NYUKI |
| 5. COSTANTINE MNEMELE | AFISA UCHAGUZI |
| 6. LADISLAUS SIJE | AFISA TEHAMA |
| 7. RUMELIUS BAKIRANE | AFISA MANUNUZI WILAYA |
| 8. AARON MAYANGA | MKAGUZI WA NDANI |
| 9. EDWARD BUGANGA | AFISA ELIM MSINGI |
| 10. ZAINAB ABDALLAH | AFISA ELIMU SEKONDARI |
| 11. HASHIM ABDALLAH | AFISA MAENDELEO YA JAMII |

SEKRETARIETI

1. JAFARI ZIADA
2. TUWEJE RWAMBO

AGENDA NA: RDC/CMT/01/10/2021/01. KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuitikia wito wa kikao hicho maalumu na kuwaeleza ni kwa ajili ya kujadili fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, Jengo la wagonjwa wa Dharura na Nyumba ya mtumishi. Mara baada ya kuyasema hayo alitamka kikao kimefunguliwa rasmi mnmo saa 2:30 asubuhi.

AGENDA NA: RDC/CMT/01/10/2021/02. MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 1,350,000,000/= KWA AJILI YA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVICO 19.

Afisa mipango wilaya aliwasisha taarifa kuwa katika mapambano dhidi ya UVICO 19 Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za mapambano dhidi ya UVICO 19 amewezesha serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupata mkopo wenye masharti nafuu kiasi cha Tshs trilioni 1.3 kutoka shirika la fedha la kimataifa (IMF) kwa ajili ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVICO 19 ili kuchangia na kufufua uchumi wa sekta zilizopata athari za kiuchumi kutokana na ugonjwa huo. Matumizi ya fedha hizi zimeelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja kwa ajili ya kuwaondolea kero katika kuzifikia na kupata huduma za afya, elimu

na miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanya biashara wadogowadogo/machinga wakiwemo wanawake, vijana na walemavu.

Katika fedha hizo Halmashauri imeidhinishiwa jumla ya **Tshs 1,350,000,000/=** katika utekelezaji wa miradi ya elimu na afya katika mchanganuo ufuatao;

- I. Vyumba 36 vya madarasa katika Shule za Sekondari. Jumla ya **Tshs 720,000,000/=**
- II. Vyumba 12 vya madarasa katika Shule Shikizi. Jumla ya **Tshs 240,000,000/=**
- III. Jengo la wagonjwa wa dharura (EMD) jumla ya **Tshs 300,000,000/=**
- IV. Ujenzi wa Nyumba ya mtumishi (3 in 1) jumla ya **Tshs 90,000,000/=** katika kituo cha Afya Ngorongo.

Mchanganuo wa fedha hizo katika utekelezaji wa miradi hiyo upo kama ifuatavyo


S/N	JINA LA SHULE	IDADI YA MADARASA	KIASI CHA FEDHA
1	MWASENI SEC	4	80,000,000/=
2	NGORONGO SEC	4	80,000,000/=
3	MKONGO SEC	4	80,000,000/=
4	UMWE SEC	4	80,000,000/=
5	KAZAMOYO SEC	3	60,000,000/=
6	IKWIRIRI SEC	3	60,000,000/=
7	MBWARA SEC	3	60,000,000/=
8	UTETE SEC	3	60,000,000/=
9	CHUMBI SEC	5	100,000,000/=
10	KIFURU SHULE SHIKIZI	2	40,000,000/=
11	MUPI SHULE SHIKIZI	2	40,000,000/=
12	SHELA SHULE SHIKIZI	3	60,000,000/=
13	NYAMIDEGE SHULE SHIKIZI	2	60,000,000/=
14	MIANGALAYA SHULE SHIKIZI	2	40,000,000/=

Hivyo wajumbe kwa ujumla yao waliridhia na kumshukuru mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kuijenga nchi kwa kukuza sekta za elimu na biashara.

AGENDA NA: RDC/CMT/01/10/2021/03: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuwasihi kujiandaa kwa ajili ya usimamizi dhabiti wa ujenzi wa miradi hiyo na kusimamizi matumizi ya fedha hizo na

kuhakikisha zoezi hilo linakamilika kwa wakati kama ilivyoainishwa katika waraka wa muongozo. Mara baada ya kuyasema hayo alitamka kikao kimefungwa rasmi saa 4:20 asubuhi.



MWENYEKITI

UMEDHIBITISHWA:



KATIBU